

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA ARUSHA YA UFUNGUZI  
WA MKUTANO WA WADAU NA WATAALAM WA AFYA  
TAREHE 18-19 JANUARI,2017 -MKOA WA ARUSHA**

**Wah. Wakuu wa Wilaya**

**Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,**

**Ndugu Makatibu Tawala Wasaidizi,**

**Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya,**

**Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha,**

**Wenyeviti wa Halmsahuri,**

**Wadau wa Afya,**

**Washiriki wote wa Mkutano huu,**

**Wanahabari,**

**Mabibi na Mabwana,**

**Bwana Yesu asifiwe/Tumsifu Yesu Kristu/Asalaam  
Aleykum.**

Awali ya yote napenda kutoa shukrani za dhati kwa heshima ya kunialika kuja kufungua mkutano huu wa wadau wa afya Mkoa wa Arusha.

Ninapenda niseme kuwa nimefurahia mwaliko huu ambao unaniwezesha kushirikiana nanyi katika suala hili muhimu katika utoaji wa huduma za Afya kwa wananchi wa Arusha na Taifa kwa ujumla.

## **Ndugu washiriki**

Lengo la mkutano huu ni kutathimini utekelezaji wa shughuli za Afya katika Halmashauri zetu na kutambua fursa na changamoto tulizonazo tuweze kuandaa mikakati ya pamoja ili kuweza kuboresha huduma za Afya ndani ya Mkoa

Ninashukuru sana idara ya afya Mkoa kwa kuona umuhimu wa kufanya mkutano huu wenye lengo la kuboresha huduma za Afya Mkoa.

### ***Ndugu Washiriki,***

Ni imani yangu kuwa mtajadili kwa kina hali halisi ya utekelezaji wa shughuli za Afya ndani ya Halmashauri zetu ili kuweka mikakati madhubuti katika kuboresha hali ya Afya katika Mkoa wetu wa Arusha.

Kama mnavyofahamu, mabadilliko ya Sekta ya Afya yanayoendelea yanalenga kuboresha huduma za Afya nchini kwa kutumia dhana ya matokeo makubwa sasa (BRN) ili kufikia malengo ya millennia . Lengo kuu likiwa ni kupunguza vifo vya watoto wachanga, watoto wa umri chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito, kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza pamoja na kuboresha afya ya mazingira na kupata maji safi na salama. Ili kufikia malengo haya serikali peke yake haitaweza, bila kushirikiana na wadau mbalimbali ambao wamekuwa na mchango mkubwa sana katika kuboresha afya za

Watanzania kwani kama tujuavyo wote “***Umoja ni Nguvu na Utengano ni udhaifu.***”

Michango yenu bado inahitajika katika kuboresha maeneo mbalimbali hasa ya miundo mbinu kama: ukarabati wa majengo na ujenzi wa vituo vipya hususani katika Halmashauri ya Longido, kutoa mafunzo ili kuwajengea uwezo watumishi kwa lengo la kuongeza vigezo ambavyo havijafikiwa, kuongeza kiwango uandikishwaji wa CHF.

Nina imani kubwa kuwa kama nguvu hizi kwa pamoja zitaunganishwa tutaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto zilizopo katika Halmashauri zetu zote ili tuweze kufikia malengo ya Kitaifa.

### **Ndugu Washiriki,**

Serikali inathamini sana mchango mkubwa unaotolewa na wadau katika kuhakikisha wananchi wa Mkoa huu wanapata huduma za afya zilizo bora.

Nina imani kuwa wadau mliopo kwenye mkutano huu mtazichukua changamoto zilizojitokeza katika kila Halmshauri ili muweze kusaidia kuzitatua kadri ya uwezo utakavyo ruhusu. Kwa wazee wangu LAIGWANANI tunawaomba mpeleke ujumbe mlioupata kwenye mkutano huu kwa jamii tunazoziongoza ili kuleta mabadiliko chanya katika kuboresha afya na ustawi wa jamii husika. Vilevile mkutano huu utatoa fursa kwa Halmashauri kujifunza kwa Halmashauri ambazo zinafanya vizuri na kuchukua changamoto za wengine kama maeneo ya kuboresha.

***Asanteni kwa kunisikiliza***